



BODI YA USAJILI WA MAKANDARASI (CRB) TAARIFA YA MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA TANO 2015 HADI 2020



Muonekano wa maendeleo ya upanuzi wa barabara ya Kimara - Kibaha Km. 19.1 jijini Dar es Salaam kutoka njia mbili hadi nane unaofanywa na Mkandarasi wa ndani Estim Construction Company Limited.

Utangulizi

Bodi ya usajili wa Makandarasi (CRB) ni taasisi ya umma chini ya Wizara ya Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano (sekta ya Ujenzi), iliyoanzishwa kwa sheria ya Bunge namba 17 ya mwaka 1997 iliyofanyiwa mabadiliko (as amended).

Majukumu makuu ya Bodi ni pamoja na;

- Kusajili Makandarasi wa aina zote
- Kuratibu shughuli na mwenendo wa Makandarasi na
- Kujenga uwezo wa makandarasi wa ndani.

Bodi, katika utekelezaji wa majukumu yake mbalimbali kwa niaba ya serikali, inayo mafanikio ya kujivunia yaliyopatikana katika kipindi cha miaka mitano, yaani mwaka 2015 hadi 2020. Mafanikio ya Bodi ni mafanikio kwa niaba ya Serikali ya Awamu ya Tano.

Mafanikio ya Bodi katika kipindi cha miaka mitano (2015 hadi 2020).

1.Usajiliwa Makandarasi.

Bodi imehakikisha inasajili Makandarasi bora kwa kuzingatia vigezo vinavyoendana na wakati tulionao ili kupata Makandarasi wenye sifa na uwezo wa kutekeleza kazi za mikataba ya ujenzi wa miundombinu mbali mbali.

Bodi imepata mafanikio makubwa katika jukumu la usajili wa Makandarasi katika kipindi cha miaka mitano kwa kuongezeka kwa idadi ya Makandarasi waliosajiliwa kutoka 8,839 mwaka 2015 hadi kufikia makandarasi 11,346 mwezi Juni 2020.

Kuongezeka kwa idadi ya Makandarasi kunatokana na Serikali ya awamu ya tano kuwekeza sana kwenye ujenzi wa miundombinu ikiwemo ya barabara,

madaraja, viwanja vya ndege, ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) na mradi wa kufua umeme katika mto Rufiji.

Aidha uwekezaji huu mkubwa katika sekta ya ujenzi ni mafanikio makubwa ya kiuchumi katika nchi yetu na umeongeza ushindani wa Makandarasi wenye sifa na hivyo kusababisha waajiri, ikiwemo Serikali kupata huduma bora zenye kuzingatia thamani ya fedha inayotumika (value for money) katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi.

2.Kuratibu shughuli na mwenendo wa Makandarasi

Bodi inalo jukumu la kuratibu shughuli za Makandarasi ili kuhakikisha kuwa miradi yote ya ujenzi inatekelezwa kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za ujenzi nchini. Ukaguzi wa miradi unasaidia kuhakiki kuwa kazi zinafanywa na Makandarasi waliosajiliwa na pia sheria za ujenzi zinazingatiwa katika utekelezaji wa miradi husika.

Bodi imepata mafanikio makubwa katika utekelezaji wa jukumu la kuratibu shughuli za Makandarasi nchini kwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika miradi ya ujenzi ambapo idadi ya miradi inayokaguliwa kwa mwaka imeongezeka kutoka miradi 2,300 mwaka 2015 hadi miradi 3,100 mwaka 2019/2020.

Uzingatiaji wa sheria umeongezeka kutoka 64% mwaka 2015 hadi 73% mwaka 2020. Hii ni ishara ya kwamba kuongezeka kwa shughuli za ujenzi kumeendana na uzingatiaji wa sheria na hii imeimarisha uwekezaji mkubwa wa Serikali ya awamu ya tano katika miundombinu bora.

Bodi imekuwa ikichukua

hatua za kisheria pale inapobainika kuwa miradi ya ujenzi inatekelezwa pasipo kuzingatia sheria za ujenzi. Kama mradi wenye kasoro unatekelezwa na Mkandarasi, Bodi huchukua hatua za kisheria kama vile Mkandarasi husika kutozwa faini. Aidha pale inapobainika kuwa mradi unafanywa na watu wasio Makandarasi, Bodi huwafikisha mahakamani watekelezaji hao pamoja na waajiri wao na ujenzi wa mradi husika kusimamishwa hadi sheria ifuatwe.

Katika kipindi cha mwaka 2015 hadi 2020,

Bodi pia imefanya zoezi la kuhakiki Makandarasi wote waliosajiliwa ili kujiridhisha kama bado wanazo sifa kulingana na madaraja walioyosajiliwa. Makandarasi ambao wamepoteza sifa za kuendelea kuwa katika madaraja waliyopo walishushwa hadi madaraja stahiki na wale waliokutwa wamepoteza sifa za kuendelea kuwa makandarasi walifutiwa usajili.

Katika kipindi cha mwaka 2015 hadi Julai 2020, Bodi imefuta jumla ya Makandarasi 1794 kutokana na makosa mbalimbali.

3.Kujenga uwezo wa Makandarasi.

3.1. Mafunzo

Bodi inao wajibu wa kuendeleza Makandarasi wazalendo kwa lengo la kukuza uwezo wao na kuwawezesha kushindana katika soko la kazi za ujenzi ndani na nje ya nchi. Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015 hadi 2020, Bodi imeboresha mafunzo kupitia mpango maalum wa mafunzo endelevu kwa Makandarasi (Sustainable Structured Training Programme - SSTP) ulioanzishwa

mwaka 2001 kwa lengo la kutoa mafunzo stahiki yanayoendana na wakati na kwa kutambua umuhimu wa kuwa na Makandarasi wenye uwezo na ujuzi wa kutosha ili kutekeleza miradi mikubwa ya miundombinu inayotokana na uwekezaji mkubwa wa Serikali ya awamu ya tano.

Katika kipindi cha miaka mitano kumekuwa na mafanikio makubwa kwa kuwa mafunzo yametolewa kwa idadi kubwa ya Makandarasi. Idadi ya washiriki wa mafunzo imeongezeka



Muonekano wa maendeleo ya ujenzi wa Daraja la Salender jijini Dar es Salaam.